

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SIMU: 025 - 2502260
Fax: 025 - 2500128



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
S.L.P. 599
MBEYA.

Barua pepe: ded@mbeyadc.go.tz

Kumb.Na. MDC/

08.04.2019

YAH: TANGAZO LA MARUDIO LA AJIRA YA MKATABA YA KAZI YA FUNDI SANIFU UMEME (*Electrical Technician*) NAFASI - 1

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya anayo furaha ya kutangaza nafasi za Ajira ya Mkataba kwa kazi ya Fundi sanifu Ufundi Umeme (*Electrical Technicians*) nafasi - 1 katika Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

1.0 FUNDI SANIFU UMEME (*Electrical Technician*) NAFASI – 1

1.1 SIFA ZA KAZI

1. Cheti cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne (IV).
3. Cheti cha Diploma ya Ufundi
4. Kila Mwombaji awe na Mdhamini atakayetambulishwa na Serikali ya Kijiji/Mwajiri.

2.0 KAZI ZA KUFANYA

- a. Kufanya kazi zote za fani ya Umeme kwenye majengo mbalimbali ya Halmashauri
- b. Kuandaa michoro ya Umeme kwenye majengo mapya na yanayohitaji matengenezo .
- c. Kufanya kazi za kutengeneza vifaa vya Umeme.
- d. Kufanya usanifu wa miradi midogo ya Umeme, kusimamia jinsi ya kufunga mashine mpya za Umeme zinazoweka kwenye majengo yote ya Halmashauri

2.1 MSHAHARA

Mshahara kwa mwezi ni Tsh. 525,000/= . (Kabla ya Makato)

3.0 MASHARTI YA JUMLA

- a. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.
- b. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe na hajawahi kupatikana na kosa la Jinai au kufungwa jela.
- c. Muombaji awe na Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) katika fani hiyo.
- d. Maombi yote yaambatishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V).

- e. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya Elimu (IV au VI), Ujuzi, Cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) na iandikwe jina nyuma.
- f. “Testimonials”, “Provisional Results” “Statement of Results” hati ya matokeo ya kidato cha Nne Havitakubalika.
- g. Mwombaji aliyestaafishwa /Kufukuzwa kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba.
- h. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- i. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 23.04.2019 saa 9.30 Alasiri.
- j. Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na yatumwe masjala ya Mkurugenzi Mtendaji (W) au kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya,
S.L.P. 599,
Mbeya.**

Imetolewa na

**Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya**